



COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD

Wednesday, 14th August, 2024

Third Assembly – Third Session
SIXTY SIXTH SITTING

*[The County Assembly met at 10:04a.m at the County Assembly Buildings]
[The Speaker (Honourable Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair]*

PRAYERS

The Speaker (Hon. Khatri): You may be seated Honourable Members. Clerk's, please confirm if we have quorum?

[Lack of quorum]

Serjeant -At-Arms, please ring the bell for 10 minutes.

[The Serjeant-At-Arms rung the quorum Bell]

Yes, Honourable Abdirahman?

Hon. Abdirahman Abdikadir: Thank you Mr. Speaker, I am just up on a point on order just seeking your clarification on point of order on quorum, whether the bell should be rung for ten minutes consecutively or it is rung and then we wait for ten minutes. I am just seeking your interpretation on that.

The Speaker (Hon. Khatri): I think if we go through Standing Order 31(2) maybe if I can read,

'If there is not a quorum present when the Chair is taken, at the time appointed for a meeting of the County Assembly, immediately after the saying of the prayer, the Speaker shall order the bell to be rung for ten minutes, if no quorum is present at the expiration of the 10 minutes, the Speaker may direct that the bell be rung for a further five minutes and if there is still no quorum present, the Speaker shall adjourn the County Assembly forthwith to the next sitting'.

So, the bell of cause shall be rung for ten minutes continuously yeah. Sergeants -At-Arms did you ring the bell for ten minutes? I think you need to ring the bell for ten minutes, so please do so thank you.

[Quorum Bell rung]

[Silence]

Clerk, please confirm if we have quorum?

[Lack of quorum]

Next Order please?

MOTION

PROVISION OF MOBILE CLINIC AT SISI KWA SISI AREA IN KIPEVU WARD

Yes, Honourable Leila Nyache MCA Kipevu Ward, please move the Motion.

Hon. Nyache: Thank you Mr. Speaker for allowing me to read the Motion on Provision of Mobile Clinic at Sisi Kwa Sisi Area in Kipevu Ward. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion;

AWARE THAT, access to healthcare is a fundamental right protected in the Constitution of Kenya under Article 43 (1) (a), which mandates the state to provide the highest standards of health to all citizens;

Mr. Speaker, FURTHER AWARE THAT, Magongo Health Centre, a Level 3 facility, is currently overburdened, serving nearly three Wards, which leads to congestion and inefficient service delivery;

Mr. Speaker, CONCERNED THAT, the current state of congestion at Magongo Health Centre results in long waiting times, inadequate patient care and increased risk of infections;

Mr. Speaker, DEEPLY CONCERNED THAT, without immediate action, the healthcare problem in Kipevu Ward will continue and affect the wellbeing of residents, especially children, the elderly and those with chronic illnesses;

Mr. Speaker, RECOGNIZING THAT, a mobile clinic at Sisi Kwa Sisi area would decongest Magongo Health Centre by providing accessible healthcare services to the residents;

Mr. Speaker, NOTING THAT, mobile clinics have been successfully implemented in other Wards making healthcare available at grass root level;

Mr. Speaker, APPRECAITING THAT, the establishment of a mobile clinic at Kipevu Ward is supported by the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya, which outlines the functions and powers of County governments in the delivery of health services;

Mr. Speaker I, therefore urge this Assembly to RESOLVE:

1. *THAT, the County government of Mombasa establishes a mobile clinic at Sisi Kwa Sisi Area in Kipevu Ward to provide immediate, accessible, and effective healthcare services to the residents;*
2. *THAT, the County government of Mombasa allocates necessary resources and funding to put up and maintain the mobile clinic for the benefit of the residents of Kipevu Ward;*
3. *THAT, the County government of Mombasa conducts regular assessment of healthcare needs in Kipevu Ward to continually improve and expand healthcare services, ensuring they meet the needs of the community.*

Thank you, Mr. Speaker. I beg Honourable (OJ) Joshua to support the Motion.

Hon. Mose: I support.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Members. Honourable Members, I now propose the question the Motion by Honourable Leila Nyache on Provision of Mobile Clinic at Sisi Kwa Sisi Area in Kipevu Ward, be considered by this Honourable House in the same terms as moved?

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Nyache, please make your contribution.

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunipa nafasi nyengine tena ya kuweza kujenga hoja hii ambayo nilioleta. Mheshimiwa Spika nimeamua kuleta hoja hii hapa katika Bunge hili ya kwamba kule kwangu Kipevu Wadi sina hospitali, na hospitali ziko lakini ziko kwa Wadi za wenzangu iko kwa Wadi ya Mheshimiwa Frankline Makanga (Hossana), kwa Wadi ya Mheshimiwa Fadhili Makarani na kwa Mheshimiwa Bernard Ogutu lakini kwangu sina hospitali na watu wangu wakiwa wagonjwa wanachukua hatua ya kwenda mpaka hizo Wadi nyengine kwenda kutibiwa; kwa mfano kama mama ataka kujifungua sana huwa wanapata shida sana kuchukua muda wa kufika mpaka kule hospitali katika Wadi nyengine. Mama unakuta anajifungulia pale njiani anapata matatizo sana na hata watoto pia kuuguwa mtoto amezidiwa labda atakikana apelekwe mara moja hospitali inabidi tena watu watafute njia ya kwenda katika hizo Wadi zingine unakuta mtoto azidiwa saa zingine mtoto anapoteza maisha hapo njiani. Mimi nimeamua kuja na hii hoja ya kwamba pia mimi niweze kupata hata kama ni *mobile clinic* ambayo nitaweza kuwekewa pale kwa sababu katika wadi yangu Kipevu Wadi hakuna ardhi lakini kuna sehemu ambazo za kuegesha magari haya Kaunti twaweza kuja tukabandikiwa hata kama ni *container* pale na madawa na madaktari ambayo yaweza kusaidia hata kama itakuwa si kulaza ni kutibu yale maradhi ambayo yatakayo kurupuka ghafla yaweza kusaidia kama hiyo ajali ama kujifungua kwa mama ama mtoto labda ameshikika na kuhara hivi yaweza kusaidia ndio kitambo tutafute njia za kwenda kama Makadara ama Port Reitz ama hospitali nyengine. Hivyo basi, Mheshimiwa Spika nimepata shida sana na wananchi wangu saa zote kuniambia ya kwamba niweze kuja huku niweze niwaombe hata kama ni hio *mobile clinic* waweze kuwekewa pale na waweze kupata matibabu.

Kwa kweli Mheshimiwa Spika sisi tumechaguliwa na watu wetu na tumechaguliwa tuje tuwakilishe hapa katika Bunge la Kaunti ya Mombasa na kuwakilisha ni kama hivi, kwa sababu huwezi kuwakilisha watu wakiwa ni wagonjwa kila siku na hata kukusikiza hawatakusikiza na hata hivyo kura kukupigia akiwa mgonjwa hawezi. Hivyo basi mimi ningeomba tu Bunge hili waweze kuniunga mkono niweze kuwekewa hii *mobile clinic* ambayo itaweza kupunguza ule msongamano wa watu wangu kwenda katika hospitali zingine kama Port Reitz ama Chaani maana yake ukifika kule pia saa zingine kumejaa tele Magogo pia saa zingine pia kumejaa tele madawa pia saa zingine hakuna pia ningeomba pia hizi hospitali zilioko ziweze kuangaliwa kwa madawa na sisi wa Wadi ya Kipevu tuweze kupata hii *mobile clinic* na sisi tuweze kupata matibabu ya karibu na pia ningeomba pia serikali Gatuzi kuna nyumba ambazo zinauzwa wanaweza kukubaliana na sisi watu wa Kipevu waweze kutununulia. Kuna zile nyumba zinauzwa za Kiswahili halafu waweze kutujengea pale hospitali yetu tuweze kupata matibabu ya karibu Mheshimiwa Spika, kwa hivyo naomba Bunge hili muniunge mkono watu wangu wa Kipevu waweze kupata hio *mobile clinic* na waweze na wao kuwa na afya njema kama wananchi wengine maana yake wamenichagua nje kuwakilisha waweze kupata afya njema, wapate elimu, wapate vibarua na wapate maendeleo tofauti tofauti, wapate taa barabarani. Mambo ni kama hayo lakini leo nimekuja kuomba waweze kupata hii *mobile clinic* na wao pia waweze kujisikia kama wananchi wengine na waweze kupata afya bora, ahsante sana Mheshimiwa Spika.

[The Speaker (Hon. Khatri) exited the Chair]

[The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani) in the Chair]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Leila Nyache. Yes, Honourable Jactone Madialo?

Hon. Madialo: Ahsante Mheshimiwa Spika. Nilivyoingia katika Jumba hili asubuhi ya leo kitu cha kwanza ambapo Mheshimiwa mwenzangu Mheshimiwa Joshua Ong'ao ambaye amekaa kando yangu hapa, kitu cha kwanza ambapo ameniambia ni kwamba tupinge hoja na akanipatia sababu zake nyingi. Ya kwamba sababu ya kwanza kuna hospitali kubwa Port Reitz hapo karibu, kuna hospitali ya Chaani pale ambapo pia ni kubwa lakini mimi nikashangaa sana ya kwamba yeye ndiye ame *second*; sasa kwa sababu hio mimi ninauunga mkono. Ahsante.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Maryam Baimu?

Hon. Baimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii mimi nimesimama kuunga mkono hoja hii iliyoletwa na mwenzangu dadangu Mheshimiwa Leila Nyache wa Wadi ya Kipevu. Kusema ule ukweli Mheshimiwa nina imani afya ni jambo la muhimu sana hata kuliko mali, hata kitu kingine kwa hii dunia; kwa hivyo Mheshimiwa anaposimama kuomba kama tutaweza kupitisha hii hoja kuweza kufanyika *mobile clinic* hata tukiangalia sisi kwa sisi hilo jina kwamaanisha tayari hilo jina hapo, hilo eneo ni watu kwamba wako na umoja na kutaka kupata maendeleo katika ile sehemu. Kwa hivyo Mheshimiwa Leila Nyache mimi nakuunga mkono ili hii kliniki, kando ya kliniki mimi ningeomba hilo wazo lako ya kwamba mfano kama itawezekana serikali ya Kaunti tuweze kununua hizo nyumba za Kiswahili ama moja ni mbili hapo maeneo ama moja ziweze kuvunjwa zijengwe hio hospitali haswa kwa sababu hatuwezi kujivunia hospitali ambayo iko kwa Wadi ya mwenzetu.

Ni vizuri hata wewe miaka mitano ikiisha unapotoka katika hili Jumba basi mojawapo ya vitu utakavyojivunia kama Mheshimiwa ni kwamba uliweza kuleta matibabu ikiwa ni hospitali. Ni vizuri zaidi ikiwa ni hio *mobile clinic* pia itaweza kukusaidia kwamba uliwafikiria watu wako wa Kipevu na ukaweza kuleta hospitali karibu na wao. Kwa hayo mengi mimi nasema ahsante sana nimesimama kuunga mkono hio hoja.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Katana?

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika, kule Barsheba kama unaelekea Bamburi kunayo *container* kwa kukosa neno zuri la Kiswahili ambalo ni la matibabu ya *mobile* na pale ninapoliona limechorwa tu ya kwamba Kaunti ya Mombasa *Mobile Clinic* lakini halifanyi kazi yeyote. Sasa ikiwa Mheshimiwa Spika maombi yamekuja yakwamba katika kata ndogo moja ndani ya Kaunti ya Mombasa inakosa mahali pa matibabu ya haraka kwa watu wa pale mahali, tutakuwa tunakosa hekima kuunga mkono hoja hii ili kitu ambacho hakina gharama. Mheshimiwa Spika ni kwamba liondolewe pale barabarani na lipelekwe Kipevu ili watu wa Kipevu watu wa Kipevu wapate kusaidika Mheshimiwa Spika...

[Applause]

Na si tu hiyo Mheshimiwa Spika, hoja hii mimi ninge kuwa nimeiona mapema labda kabla kuungia hapa ningeongeza kusema kwa kuwa Katiba yetu tuliyopitisha, 2010 inauunga mkono sana mfumo wa Ugatuzi. Ni lazima serikali ya Kaunti ya Mombasa iwe kwa njia yeyote ile itatafuta kiwanja na hii iwe ni natija tu ya muda ya *mobile clinic* lakini kutafutwe kiwanja kutoka kwa mtu yeyote serikali ya Kaunti inunue na kuweze kuwe na hospitali pale; na kwa hilo Mheshimiwa Spika niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Leila Nyache kwa kufanya kazi baadhi ya kazi zilizomleta hapa kupitia kwa watu wake kuwatetea ili waweze kupata urahisi katika matibabu wanapokuwa wagonjwa. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Mohamed?

Hon. Mohamed Hassan: Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipatia hii fursa na nina furaha baada ya muda kuweza kuchangia katika hoja iliyoletwa na Mamangu kuhusiana na mambo ya matibabu ama afya katika eneo lake. Nilikuwa niuunge hoja hii lakini inanilazimu nipinge kama *container* litatolewa kwangu lipelekwe kwake nitapinga tu, nashangaa anayetoa hoja ya kutolewa *container* kwangu ana hospitali ya daraja la 5 sijui yaenda 6 yafanana na Mombasa Hospital ama Makadara lakini *container* langu linamuasha; sasa si ni kuchora sufuri na kufuta ziro? Litolewe kwangu lipelekwe kwake halafu kwangu kuna wakali kwanza pale watu watatibiwa wapi? Mapanga ni mingi sana, lile *container* ndugu yangu Mheshimiwa Allen Katana, 1GB halina mambo mengi lina *plaster*, *spirit* na pamba sisi twashughulika tu na vipanga peke yake sasa likitolewa si watu watakufa?

[Laughter]

Kwa hivyo Bwana Spika napiga hoja hii. Ahsante sana.

[Applause and Laughter]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Frankline Makanga?

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika. *From the onset I wish to put records straight that I support the Motion. This is in accordance to Schedule 4 Part (II) of the Constitution of Kenya 2010 that outlines the County health services to be a function of the County government and amongst those services Mr. Speaker it includes the County health facilities and pharmacies, ambulance services, promotion of primary health care and all those that are listed down there. Honourable Speaker while I do support the Motion, I would suggest more recommendations to the mover of the Motion and maybe in Kiswahili Mheshimiwa Spika ni kwamba katika neno ambalo limetumia la mobile clinic inamaanisha ya kwamba ni kitu ambacho hakitakua kimewekwa mahali inapeana hizo huduma, inamaanisha kwamba leo iko sisi kwa sisi kesho iko Mainland, kesho kutwa imeenda Kwa Hola na inaenda kumalizia Fox Inn. Kwa hivyo mimi nikisema kwamba labda kwa sababu the intent and the motive of having this Motion Honourable Speaker is to devolve further the health functions so that the people of Kipevu Ward ambayo ilizaliwa kutoka Wadi ya Chaani pia wapate huduma.*

Mheshimiwa Spika nimetangulia kusema nauunga mkono lakini jina ambalo limetumika ya kuifanya iwe mobile labda wangesema container ya kwamba kwa sababu hawana nafasi ya kuiweka ingekuwa na urahisi wa kueleweka, lakini tukisema mobile, inamaanisha a group of health care workers wanakuja pale wanapeana huduma and because they are mobile as the term says, then they move to another area. Mimi kile ningeomba ni kwamba Mheshimiwa Spika, inapopitishwa hoja hii, ipitishwe na mabadiliko ya kwamba, awekewe kama ni hiyo temporary infrastructure ambayo ni kama hizo container ili iweze kupeana huduma nimemsikia katika maombi yake kwamba wamama wakitaka kujifungua, hawana mahali pa kujifungua. Labda nimwambie kwamba kiwango hichi cha afya ama this level of facility kulingana na sheria za afya, hawaruhusiwi wazazi kuzaa pale. Kwa hivyo hiyo pia ieleweke na mimi ningeomba nikisimama na Mheshimiwa mwenza ni kwamba Kipevu watu wanazaana Mheshimiwa Spika, watu wanazaana, watu wanafanya hiyo shughli kabisa! Hiyo inamaanisha watoto ni wengi na wazazi ni wengi kwa hivyo Mheshimiwa Spika, ajengewe hospitali ya kisawasawa.

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Frankline, there is another Member who is up. Honourable Joshua what is it?

Hon. Ong'ao: Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa ambaye anaongea sasa hivi, atuambie wale wanazaana kule wake ni wangapi na data ametoa wapi, isije akasema mambo ambayo hakuna.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Frankline, proceed.

Hon. Makanga: Mheshimiwa Spika, unajua labda Joshua Ong'au ambaye ni mwakilishi Wadi wa Jomvu kuu alidhani nitasema kwamba pia watoto wake wako kule, hiyo sio sababu ya mimi kusimama wanaweza kuwa wamo.

Ndio maana Mheshimiwa Leila akamchagua kuunga mkono hilo sitasema na lisiwekwe katika rekodi za Bunge hili lakini nikiselelea na mjadala ambao nilikuwa nasema na hayo ni maneno ambayo Mwakilishi Wadi wa Kipevu anae wajua watu wake na uwezo wao wa kuzaana, maana ameyasema hapa watoto wanataabika wamama wakitaka kujifungua wanapata shida, natumia maneno aliyo yanukuu Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo mimi ningeomba ni kwamba Bunge hili tumsaidie Mheshimiwa huyu aweze kupata hii hospitali ambayo itaweza kuangazia yale yote ambayo ameyasema kwa sababu Kipevu ni kubwa, wananchi ni wengi na inapobidi kwamba watembe usiku kuenda kwa hospitali nyengine. Mheshimiwa Spika wanataabika kwa hivyo namuunga mkono lakini isiwe tu mobile kwamba inakuja na ikienda, awekewe *facility* ambayo itawahudumia wale wananchi wa Kipevu, wapate huduma ambazo zina *meet the standards* ambazo ziko katika katiba ya Kenya na hayo Mheshimiwa Spika nimeyasema kama mjuzi katika taaluma hii. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu): Yes, Honourable Florence?

Hon. Kachumbo: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity, I would like to thank God for the gift of life. I would like to congratulate my fellow colleague for bringing such a good motion to the House. It is such an admirable thing when you see a leader considering the people in mashinani. We see Honourable Leila Nyache has seen a major concern to the people of Kipevu ward and she is performing very well being one of her major duties which is representation and which she is representing her people here and I would like to urge the House to support her and the County government at large by gathering resources and building a nice hospital, I wouldn't say a clinic because am sure we will be able to find land and help the people of Kipevu Ward, thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Milka?

Hon. Ngare: Thank you Mr. Speaker, I rise to support the Motion and to associate myself with the sentiments of especially Honourable Makanga on giving...

[Interruption]

Mr. Speaker protect me from the Honourable Members to my right.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Fatma, consult on low tone. Proceed Honourable Milka.

Hon. Ngare: Thank you. Honourable Leila has seen the need of her people missing on health services but if it is to make more meaning as Honourable Makanga has said she needs a better facility than a mobile clinic so that the people of Kipevu Ward can have access to better services as she has put it so let us support the Motion but also upgrade, so that the facility there will be more meaningful to offer services to the people of Kipevu so I do support the Motion. Thank you, Mr. Speaker.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Hamid?

Hon. Hamid Mohamed: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mimi nimesimama kuchangia Mswada huu wa Mheshimiwa Mwenza wa Kipevu na sababu kuu ni moja ama mbili. Ya kwanza, tunapokuwa na vituo vya huduma za afya kwenye Wadi zetu tunapunguza kimombo *congestion* kwenye zile sipitali za level 4. Kwa hivyo hiyo ni sababu ya kwanza na naona ni muhimu sana ikiwa tutakuwa na kliniki kwenye Wadi yake ya Kipevu. Pili, hii huduma ya afya ambayo dada anaililia hapa si kubwa, hizi ni zile tunaziita *emergency cases* yaani kama mtoto amekatika anaweza kuangaliwa na kushonwa pale kwa pale na kama mama amefika wakati wa kujifungua, basi pia anaweza kuhudumiwa. Lakini hiyo ni nafasi ya wagonjwa na wakaazi wa hapo kuhudumiwa mara moja na kwa *discharged* kurudi nyumbani, hivyo basi ninaunga mkono moja kwa moja hoja hii ya Mheshimiwa wetu wa Kipevu.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Mbaya?

Hon. Hamisi Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii. Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama kuunga mkono hoja hii na kwa hakika kabisa nikiangalia kutoka nana mazingira tunayoishi, sioni sababu ya mimi kupinga swala hili kwa sababu Mheshimiwa Spika, maswala ya afya, hatauwe tajiri kiasi gani kama kutakuwa na matatizo ya afya utajiri wote utapotea Mheshimiwa Spika. Kwa sababu hizo na nyengine Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono hoja hii kwa asilimia thamani kwa mia. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Fatma Mote?

Hon. Fatma Swaleh: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunipa fursa hii. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi pasi na kizuizi kwa siku hii ya leo sote kuwa hapa. Mheshimiwa Spika, kama unavyojua Waheshimiwa wa Jumba hili huwa wanaleta hoja muhimu, hoja nzuri, hoja za kusaidia wananchi wao. Mheshimiwa Spika, kabla sijasema naunga ama napinga naomba uniruhusu kidogo tu niweze kuchangia kabla sijaamua kama naunga ama napinga. Jambo la kusikitisha ni kwamba hoja zinaletwa ndani ya hii Nyumba; kule nje mashinani wananchi wanafikiri sisi tunakuja tu hapa tunabweka bweka alafu tunaondoka. Mheshimiwa Leila ameweza kuleta hoja nzuri sana ndani ya hili Jumba kulingana na watu katika Wadi yake na mahitaji katika Wadi yake, cha kusikitisha ni kwamba, leo hii hoja ya Mheshimiwa Leila ikipita utekelezaji itakuwa hakuna. Mimi niko katika Kamati ya Afya lakini malalamiko huko nje ni mengi kwamba watu wanakwenda hospitali hakuna madawa Mheshimiwa Spika...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Fatma, there is a point of order have your seat please?

Hon. Makanga: Mheshimiwa Spika, Kanuni zetu za Kudumu zinazuia matumizi ya maneno makali, sasa aliyekuwa anazungumza ni Mwenyekiti wa Kamati ya afya, Naibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya afya. Mheshimiwa Spika, sijui kama ni sawa yeye kusema Waheshimiwa wanakuja hapa kubweka bweka kwa sababu ni mbwa peke yake wanaweza bweka Mheshimiwa Spika. Sasa labda kwa sababu yeye ni Naibu Mwenyekiti labda ametupima akatuona sisi sote hapa ni mbwa ama vipi Mheshimiwa Spika!

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Kushe, please reply.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika, kusema ni kwamba nimesema kweli kwamba tunaonekana tunabweka bweka kwa sababu yale yote tunayo zungumza hapa, hayatekelezwi ndio maana kule nje wananchi wetu wanajuwa sisi huja humu ndani tuka bweka, maana yake hakuna. Mheshimiwa Spika wacha nikupe mfano mdogo, tulisema kwamba tulipitisha mgao wa basari tukasema hakuna mototo anatakiwa abakie nyumbani lakini hivi sasa ukizunguka mitaani utaona watoto wako nyumbani wakiulizwa wanasema hawana karo ya shule. Mheshimiwa Spika, naomba unikinge na daktari haijulikani ni daktari wa kutibu magojwa gani kwa hio naomba niendeleo kwa sababu Mheshimiwa Leila ameleta hoja nzuri...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): The Chairman Education is up, so let us here from him, yes Honourable Ibrahim?

Hon. Omondi: Thank you Mr. Speaker. I stand on point of information to this House. Mr. Speaker, indeed it is very sad, it is uncouth, it is barbaric for a respected Member and a senior Member of this Honourable House to utter words which are likely to demean the function and the character of the Members of a County Assembly the respected Members and hardworking Members of this County Assembly. Mr. Speaker...

[Applause]

Mr. Speaker, I am saying that because we are up to...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Ibrahim, go to your point because you were up on a point of information.

Hon. Omondi: Yes, Mr. Speaker I am informing the Member who was...

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Then be precise please.

Hon. Omondi: Mr. Speaker, I am informing the Member who was up to avoid using words which are likely to demean the character of Members in this particular words House Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Which particular words?

Hon. Omondi: Mr. Speaker, words like *kubweka bweka* we know the reason we are here; we are very objective and we are performing our duty....

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Ibrahim...

[Interruption]

Hon. Omondi: It's a matter of implementation Mr. Speaker. Implementation does not fall under this House it falls under Executive Mr. Speaker.

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): We have heard you Honourable Ibrahim take your seat. Honourable Fatma please withdraw the word *bwekabweka* and proceed.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Withdraw the word, *bweka bweka* because it is not a parliamentary language, please. Withdraw that word and proceed.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika kwa heshima yako! Mheshimiwa Spika lakini itakuwa unanihujumu Mheshimiwa Spika!

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): It is with respect of the House!

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika kwa heshima yako! Mheshimiwa Spika narejelea tena! Mheshimiwa Spika kwa heshima yako lakini Mheshimiwa Spika utakuwa wanihujumu Mheshimiwa Spika nimeomba samahani...!

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Fatma, just withdraw that word and proceed.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika kwa unyonge nimeomba samahani Mheshimiwa Spika lakini kwa kusema la ukweli...!

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Just withdraw that word.

Hon. Fatma Swaleh: Nishasema samahani Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Sawa samahani lakini sema kuwa nimeondosha kwa sababu tuko na *Hansard records* ondoa lile neno ambalo ulilokuwa umelitamka kuhusu kuwa Waheshimiwa wanabweka bweka. Tafuta neno mbadala ambalo halitakuwa limewaumiza Waheshimiwa.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika naomba samahani. Na nasema tena Mheshimiwa naomba samahani naondoa hilo jambo la *bwekabweka* kwa sababu Mheshimiwa Spika sisi hapa tunakuja na hoja nzuri.

Lakini hakuna utekelezaji na kwamba hakuna utekelezaji na sisi wenyewe tunanyamaza. Mheshimiwa Spika ukumbuke wewe na mimi tuliingia hapa tukaapa na msaafu ikiwa tutazungumza maneno na hayatekelezwi hio itakuwa tunaumiza ama tunahujumu waliotupigia kura Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika dadangu Mheshimiwa Leila amekuja na hoja nzuri sana lakini mimi nasikitika utekelezaji hautafanyika. Mheshimiwa Spika mimi ni Mwenyekiti mdogo wa Afya kama alivyozungumza Mheshimiwa mwenza ukizunguka katika ma hospitali mengi hakuna madawa haimaanishi kwa kuwa mimi ni Mwenyekiti mdogo wa Afya Mheshimiwa Spika nisiweze kutetea watu wangu. Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa hayo machache.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you.

Hon. Madialo: *[Inaudible]*.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Order! Order! Honourable Madialo Order! Honourable Mwaka Bakari.

Hon. Mwaka Bakari: Ahsante sana...

[Silence]

Hon. Mwaka Bakari: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii. Kwanza nipende kumshukuru Mheshimiwa Leila kuweza kuleta hoja hii ambayo kwamba ni hoja muhimu sana. Kwa sababu binadamu Afya ndio muhimu ndio jambo la kwanza katika mwanadamu na Mheshimiwa Spika Mheshimiwa Leila yeye ameonolea kwa mtizamo wake ili aweze kusaidia wananchi wa Kipevu kwa ajili ya kwamba ni mbali na hospitali zile ambazo ziko pale. Ndiposa Mheshimiwa Spika akaona alete hoja hii ya kuweka *mobile clinic* ama tunasema ni *container* manake ni *container* tunatumia neno *mobile* lakini si *mobile* ni *container* kwa kurahisisha mwendo wa hatua ndefu ya wananchi kwenda hospitali kupata huduma. Kweli Hospitali kama hii ni ndogo lakini italeta natija na itaweza kusaidia mwananchi yule ambaye kwamba hawezi kufika kule Hospitali kubwa. Kwa sababu ya hali kila kitu siku hizi ni hatua ni pesa. Pengine ambapo anakaa ni mbali na Spitali ile kubwa ataweza kupata usaidizi pale kwenye Hospitali ile ndogo. Nimetoka pale kwangu kukaa nikaja kumshauri hapa kuwa umeleta hoja hii, je ardhi iko? Akaniambia ardhi iko. Ndiposa kuwa mimi naunga mkono jambo hilo kuweza kupointiwa hatua hio ya kuwekewa *Container*. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Nyota.

Hon. Hamisi Nyota: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Mheshimiwa Spika kabla sijaingia kwenye kuchangia kwenye hoja hii Mheshimiwa spika ningependa jambo moja kidogo tulieke wazi pia. Dadangu Mheshimiwa Fatma Swaleh Mote ambaye ni MCA wa Wadi ya Kadzandani amejaribu kupitisha ujumbe kwenye Jumba hili lakini Waheshimiwa kadhaa wakajaribu kupinga ama kukataa kusikia huo ujumbe, ulikuwa una manufaa gani lakini nilinukuu yale machache aliyotaka kuongea. Mheshimiwa Spika, kusema kweli Jumba hili lapitisha hoja nzuri sana ambazo zaisaidia watu wetu kule mashinani lakini hoja hizo huwa haziendi mahali ama hazitekelezwi ndio hiyo ilikuwa Mheshimiwa Fatma Swaleh alikuwa anajaribu kuambia Jumba hili kuwa huu Mswada ni mzuri.

Mswada huu umeletwa hapa ili kusaidia jamii yetu kule mashinani lakini utekelezaji wake haufanyiki Mheshimiwa Spika ndio maana akasema akasimama ili kupitisha huo ujumbe. Mheshimiwa Spika...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Nyota, there is a person who is up! Honourable Frankline...

[Interruption]

Hon. Hamisi Nyota: Honourable Speaker, I do not want to be informed.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Have your seat Honourable Nyota.

Hon. Makanga: Mheshimiwa Spika ni jambo la kutamausha labda nilijuze Jumba hili kwamba ni kama hatujui majukumu yetu kwa sababu ni aibu yale yanayosemwa na mwakilishi wadi Hamisi Nyota ambaye ni Naibu Mwenyekiti wa Kamati ya *Public Accounts and Investments* aje hapa alalamike kwamba hayafanyiki na hao ndio wanakaa wakiangalia pesa zilivyotumika katika Bunge hili. Na anapo lalamika hakuna siku ambayo amewahi kuja katika bunge hili akasema kwamba jamani pesa zatumika lakini yale yanayofaa kufanyika hayafanyiki wasije hapa Mheshimiwa Spika kuanza kulialia hapa wakati wao wanafaa kuwa wamefanya kazi wale wote wakiwemo Naibu Mwenyekiti wa Kamati ya Afya Mheshimiwa Spika badala ya waje hapa kulalamika wawaambie wananchi wa Mombasa wanapokaa katika vyeo hivyo na viti hivyo wamefanya nini kuhakikisha kwamba afya, madawa na wafanyikazi wanapata haki zao katika mji huu wa Mombasa. Ahsante Mheshimiwa Spika.

*[The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani) exited the chamber]
[The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir) in the Chair]*

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, I am meant to understand that you were on the floor.

Hon. Hamisi Nyota: Yes, I am on the floor. Thank you, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes proceed.

Hon. Hamisi Nyota: Mheshimiwa Spika, mimi nimeshtuka sana wakati tunajaribu kusawazisha mambo ambayo yanatuathiri sisi hapa lakini kuna...

[Interruption]

Tulia! Tulia Mheshimiwa bado tulia tulia Bwana Spika please protect me from the young fellow.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Please proceed just ignore him.

Hon. Hamisi Nyota: I know he is afraid to be denied bursaries! Mheshimiwa Spika kusema kweli hili Jumba kama alivyosema Mheshimiwa Hossana hadi sisi hatujui majukumu yetu! Lakini sisi twajua majukumu yetu vizuri sana Mheshimiwa Spika; tumepitisha hoja hapa na kuna Kamati ya Utekelezaji ambayo yatakikana ifwatilizie hizi hoja zetu mpaka zitekelezwe kule mashinani Mheshimiwa Spika kile ambacho Mheshimiwa Fatma Swaleh Mote alikuwa anajaribu kuwaambia hili Jumba ni kuwa tukipitisha Miswada mizuri ambayo inafaidi watu wetu kule mashinani yatakikana itekelezwe ili faida iwafikie. Isiishie kwenye hewa na hio ndio ujumbe ambao Mheshimiwa Fatma Swaleh Mote alikuwa anataka kujulisha Jumba hili na hakuna ubaya, hakuna chuki hakuna chochote juu ya hiyo Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo nataka akae akijua kuwa Mheshimiwa yuko huru kuja kwenye hili Jumba na kuongea jambo ambalo ywaliona haliko sawa. Kwa hivyo kama yeye anasimama apinge ama akosoe lakini Mheshimiwa ana haki ya kusimama kwenye Jumba hili na aongee! Mheshimiwa Spika, ilikuwa nachangia kwenye hoja yangu kusema kweli hii hoja ambayo imeletwa na dada yangu wa Kipevu Mheshimiwa Leila Nyache ni hoja nzito, nzuri na yenye manufaa kwenye jamii yetu lakini mimi pia nataka nijulishe Jumba hili kuwa nishawahi simama mara moja kwenye hili Jumba na Taarifa kuuliza hali ya madawa ya hospitali ya Ziwa la Ng'ombe. Kwa sababu nakumbuka...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Order! Order!

Hon. Hamisi Nyota: Nakumbuka miezi kadhaa baada ya hapo ilikuwa tumeenda kule Port Reitz tukiwa na Gavana, tukiwa na viongozi wengine na tuka *flag* madawa ili yaende kwa hospitali nyanjani lakini baada ya hapo nilikuja gundua kuwa Ziwa la Ngombe hospitali haikuwa na madawa nikaja hapa kwenye Jumba hili nikajaeka statement ya kuwa nataka kujua hali ya madawa ama kiwango cha madawa ambacho kilipelekwa Ziwa la Ngombe hospitali. Mheshimiwa Spika mpaka wa leo sijapata hayo majibu Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika swala la Afya ni swala ambalo latakikana na sisi kama viongozi tusimame tulipigie upatu ili wananchi wetu wapate faida Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo mimi namsifu dadangu Leila Nyache kwasababu yeye yuwajua kuwa hili ni swala la Afya ni swala zuri na litafaidi watu wa kwao kule na nataka tulivalie njuga hili swala Mheshimiwa Spika kuwa tukipitisha mswaada hapa ambao una manufaa kwa watu wetu kule nyanjani basi sharti litekelezwe Mheshimiwa Spika. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you. Fatma Kushe I am meant to understand you have already made your contributions.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Are you on a point of Order?

Hon. Fatma Swaleh: I want to inform the House.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Please inform.

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika wajua inasikitisha sana kwa Mheshimiwa kumuona Mheshimiwa mwenzake anaongelea kitu cha maana kwa kuwa anaogopa kunyimwa basari ndio anaanza kujitetea ili salamu zisifike kwa mtu mhusika. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika tukija hapa mimi nimekuja hapa mabosi wangu ni wa Kadzandani na ikiwa nimezungumza jambo Mheshimiwa mwenzangu asiwe na wasiwasi kwamba ataweza kunyimwa basari na aliweza kuchaguliwa na wananchi wake Mheshimiwa Spika.

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Kushe...

[Interruption]

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika! Mheshimiwa Spika! Mheshimiwa Spika...!

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): You are out of Order!

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika naomba...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): You are out of Order!

Hon. Fatma Swaleh: Mheshimiwa Spika naomba manake Mheshimiwa ameweza kuniingilia sana.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Kushe you are out of Order!

Hon. Fatma Swaleh: Lakini ndio nishasema.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): You are supposed to inform the House and not to attack the Member!

[Loud consultations]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Both of you can seat down. Please!

Hon. Fatma Swaleh: I am informing the House.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Which House are you informing? Just take your Seat. Just take your Seat please! Yes, Honourable Madialo I can see you are cheering. What exactly are you cheering on? And clapping? You might also inform the House.

Hon. Madialo: Honourable Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes?

Hon. Madialo: Honourable Speaker, I am standing in support of my good friend Honourable Frankline Makanga. You gave me a chance so allow me kindly that...wacha niseme kwa Kiswahili ndio itokee vizuri. Mheshimiwa Makanga ameruhusiwa kujitakasa na Mheshimiwa Makanga jitakase kabisa. Jitakase kabisa mpaka ukionekana kule wakupatie lollipop...

[Laughter]

Maana tumechafuliwa jina huko mimi na wewe ya kutosha. Jitakase!

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Order! Order! Honourable Members. Do you want to defend yourself Honourable Makanga please do so. I will give you the chance to defend yourself please do so.

Hon. Makanga: Mheshimiwa Spika nanyang'anywa kifaa ambacho...Okay sawa. Mheshimiwa Spika nasikia kuwa leo kuna ibada ya utakaso. Kwa sababu wajua huyu ni askofu lakini hapa nafikiri tumekuja kupitisha hoja na sheria za Bunge hii. Sasa haya maswala ya utakaso, mara nasikia basari Mheshimiwa Spika mimi sidhani kama nishamaliza kusoma na kama sihitaji basari ati nisome nafikiri zile elfu hamsini ambazo tumeskia zinapeanwa ni za wale ambao wanaenda kuanza Mheshimiwa Spika kwa hivyo masuala ya basari na ibada ya utakaso nafikiri Mheshimiwa Spika *they are out of Order and you need to give directions so that they remain relevant to what is before the floor of the House.* Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Ok. Now that you have responded, I think that matter is closed. Yes, Honourable Ibrahim. Please make your contribution?

Hon. Omondi: Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker, thank you for the opportunity once again...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Ibrahim, just to advise you, you're not allowed to read from a written statement, or a written speech...

[Laughter]

Hon. Omondi: I'm not reading, Mr. Speaker! I'm not reading! I'm not reading anywhere I am just trying to express myself Mr. Speaker. Mr. Speaker first of all before I actually talk about the motion I would like to bring this matter to an end. Mr. Speaker, Honourable Kushe (Fatuma Mote) did speak here on this floor, Mr. Speaker, and I think sometimes it is very, very important for the Honourable Members in this House to be very objective. Mr. Speaker, we do not want to behave... Mr. Speaker, some of the...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Kushe?

Hon. Omondi: Mr. Speaker, sometimes we have visitors who come to this particular House, Mr. Speaker, and see how we are actually articulating issues in this particular House, Mr. Speaker. The reason why...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Fatuma!

Hon. Omondi: I need to be protected, Mr. Speaker, from Honourable Members. Mr. Speaker, one word can burn this House and one word can denature and destroy the Members, all members of this County Assembly Mr. Speaker these days, media is very sensitive, Mr. Speaker. Because, Mr. Speaker, I know myself...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Ibrahim please just contribute to the Motion now?

Hon. Omondi: Yes, that is why, Mr. Speaker, I was saying that the Member wanted to pass a point but the way she passed it was not right...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Ibrahim, are you responding to the Member?

Hon. Omondi: No, I am just trying to...She was supposed to address the executive, not the Members. Members, do not implement they are only here to do their roles and then the other side are the ones supposed... Not the Members. We do not *bweka bweka!* Mr. Speaker, we come here to articulate important issues in this particular House! Being the Chairman of education, I cannot be allowed to fall under the circle of *bweka! bweka!* up, wake up, Mr. Speaker.

[Applause]

Mr. Speaker, as I go back to the Motion today, as I said and I repeat yesterday that any Motion that will come in this House touching on matters of health, education, unemployment, and even the youth I will be the first one to support. Mr. Speaker, the mover of the Motion by the power that she was given by her people in Kipevu Ward, Mr. Speaker...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Ibrahim, you are confusing me. You are talking about Honourable Leila?

Hon. Omondi: Leila Nyanze...

[Laughter]

She is the one who brought the Motion, Mr. Speaker, and that is what I am talking about.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Leila who?

Hon. Omondi: Leila Nyanze...

[Laughter]

Mr. Speaker, what is the problem? Mr. Speaker, I want to be protected.

[Applause]

It does not matter Mr. Speaker. Where I come from, pronunciation!

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Milka?

Hon. Ngare: Mr. Speaker, with all due respect I think Honourable *Bomoa* (Ibrahim) is being harassed by this House including the Speaker himself. That is mother tongue dialect. Please allow him to continue saying Leila Nyanze, because that is the best he can do. Thank you, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): *(Laughing)*...I am not harassing Honourable Ibrahim, I'm just...

[Interruption]

Hon. Omondi: Thank you, Honourable Member, Chairs of Chairs, for that protection. I was just trying to stress or emphasize a point on this particular Motion. Mr. Speaker, before I was interrupted by the House, Mr. Speaker. Mr. Speaker, sometimes as Changamwe Sub-County, we are very proud. We are very proud, Mr. Speaker, for having this lady as a member of County Assembly of Kipevu Ward among the men...

[Applause]

Mr. Speaker, it is very rare to find such iron ladies like Leila Nyanze...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Ibrahim, you are spending most of your time showering praises at the Honourable Lady instead of contributing to the Motion. You have 30 seconds to wind up.

Hon. Omondi: Mr. Speaker, do not harass me!

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): 30 seconds!

Hon. Omondi: Mr. Speaker, health matters are very important as you can go through the prayers that she has requested; that actually there is a need to put up a Level 3 health centre in her Ward. It is indeed true because Kipevu Ward, Mr. Speaker, Kipevu Ward. My Ward neighbor Kipevu Ward and sometimes I do a walk. Indeed, it is very important that they need actually a health centre in that particular place. Mr. Speaker, I want to talk something touching on allocation...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Ibrahim, I'm afraid your time is up! Thank you very much for your contribution.

Hon. Omondi: Mr. Speaker, thank you. I stand to support.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Be blessed. Yes, Honourable Maimuna?

Hon. Maimuna Salim: Ahsante Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono Hoja hii ya *Mobile Clinics* ambayo Mheshimiwa Leila ameweza kuileta hapa. Mimi ombi langu kubwa kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Leila kwa kuweza kufikiria watu wake wa Kipevu, kwa sababu sote tuko hapa tumetumwa na watu wetu tuje tuwawakilishe na yale ambayo tunaona ni mazurui kwa watu wetu ni sawa tuyaleta kwa Bunge. Lakini mimi masikitiko yangu makubwa nitasema kuwa sisi tumekuwa kama simba sarakasi!

[Applause]

Sisi tumekuwa kama simba sarakasi kwa sababu tunazungumza hapa, tunapitisha *Bills*, tunapitisha *Motions* yaani tunafanya kazi yetu lakini ya mwisho ya *ku-oversight* hatuifanyi. Hatuifanyi! Yatakikaniwa tuwe watumishi wa watu ki kwelikweli, kwa sababu lawama zimekuwa nyingi sana mitaani, nyingi kwa walio tuchagua na wanaona sisi tunafanya lakini kwa upande wapili wa *Executive* hawafanyi. Hawafanyi! Kwa hiyo safari hii tunaomba Bunge hili yule anayepiga kelele Mheshimiwa safari hii avae nguo tusimame tuweze kuhakikisha tumefanya kazi ambayo imetuleta katika Bunge hili. Mchezo miaka miwili sasa, michezo iishe watu waumane, watu wafanye kazi kwa sababu baada ya hapo utaingia wewe kama MCA kwa Wadi yako uombe kura utashindwa na kusema ni gani? Kwa sababu Mheshimiwa Spika kusema la ukweli tukilala tatalaliwa ndio tukilala tatalaliwa na mimi nimeona hatuendi sawa. Kwa hivyo mimi nimesema...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Maimuna, I do not think that is a parliamentary statement to make. Just refrain from that please?

Hon. Maimuna Salim: Mheshimiwa Spika, mahali tunakanyaga tunakanyagwa! Mahali tunakanyaga Mheshimiwa Spika, misemo ya Kiswahili ni mingi mizuri yenye mafunzo kwa hiyo ukiyafuatilia utaweza kufaidika. Kwa hiyo tunakanyagwa na inatakikana pia sisi tukanyage, kwa hiyo mimi ninaomba Jumba hili zile Kamati husika waanze kuchukua zile *Motion* ambazo tumeweza kuzipitisha na wakae wazikague tuwaite idara baada ya idara tuangalie tutapelekana vipi ili mwananchi aweze kuona kwamba wakati umefika wakutoa kucha zetu. Mheshimiwa Spika ninaunga mkono.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Leila you my now respond the Motion?

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa ruhusa mara ya pili. Mheshimiwa Spika nataka niwapongeze sana waheshimiwa wenza na kuwashukuru kwa kuunga Hoja hii mkono ambayo nimekuja nayo hapa siku ya leo. Hoja hiyo ni ya kuhitaji niweze kupata *Mobile* ama *Container* ya madawa na madakitari katika Wadi yangu. Mheshimiwa Spika nimesikia hapa watu wakisema kwamba ama wakizungumzia swala la jina langu nami jina langu ni Leila Nyache. Nataka nimueleze Mheshimiwa mwenza hakukosea kulingana na *pronunciation* yake mimi nimeelewa kwa hivyo isiende zaidi ya hapo, *Bomoa* yuko sawa. Mheshimiwa Ibrahim Bomoa yuko sawa kabisa. Jambo lengine Mheshimiwa Spika sisi hapa waheshimiwa tumechaguliwa na wananchi na hizi ndizo kazi zetu ambazo zimetufanya tuje hapa Bungeni kuweza kuwakilisha wananchi wetu na wananchi wakiona kama hivi tumeleta kitu kama hichi kwa Bunge; kwa mfano, mimi Mheshimiwa Leila Nyache MCA wa Wadi ya Kipevu nimeleta Hoja Kama hii ya kuomba *Container* katika Wadi yangu, kwa kweli wataweza kuingia imani sana kwa sababu hawana nini? Hospitali lakini yote hayo nawashukuru Waheshimiwa wenza kwa kuniunga mkono na mimi nataka niseme tu Serikali ya Kaunti waweze kinifikiria kwa jicho la huruma na waweze kuniletea hiyo *Container* katika Wadi yangu pamoja na madawa na madakitari kama vile inavyosemekana hospitali hazina madawa. Hospitali pia ziweze kupewa madawa ziweze kuletewa madawa. Hospitali zilioko ambazo zinatusaidia kwa sasa ziwezekupata madawa na vifaa na mimi pia wawezekuniletea hiyo *Container* ikiwezekana niko na nafasi ya kuweka hiyo *Container* na pia ardhi iko kama wataamua kunijengea kabisa kuna nyumba pale nimetangulia kusema zinauzwa tutaweza kushikana na Idara niweze kuwaelezea na niwaonyeshe na niwaelezee niwapi waweze kununua ile ardhi ama zile nyumba na waweze kunijengea hospitali. Lakini kwa sasa kabla hiyo mikakati yote ningeomba niweze kuekewa hiyo *Container* na madawa na madakitari, watu wangu waweze kupata afya bora kama wengine. Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Ahsante Waheshimiwa wenza. Ahsanteni yote. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you. Honourable Members I now put the question...

[Interruption]

Honourable Ibrahim, the Speaker is on the floor and you are standing, that is gross misconduct! Honourable Members, I now stand to put the question that the Motion by Honourable Leila Nyache on provision of mobile clinic at Sisi Kwa Sisi Area in Kipevu Ward is adopted by the House in the same term as moved?

[Question put and agreed to]

The Motion by Honourable Leila Nyache on provision of Mobile Clinic at Sisi Kwa sisi Area in Kipevu Ward is adopted by the House. Yes, Clerk?

ADJOURNMENT

This House stands adjourned until Wednesday, 14th August, 2024 at 2:30p.m. Thank you.

The House rose at 11:20a.m.